SHULE YA SEKONDARI PUGU

S.L.P. 9090
**DAR ES SALAAM**
Tarehe……………………..

Simu:**0713-564051**
**0682-008720**
**0767-054942**

Mzazi wa -------------------------------------------------------------------
S.L.P. ……………………………………..

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI PUGU HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM, MWAKA 2026**

1. Ninafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha **KWANZA** katika shule hii mwaka **2026**

   Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **……………………………** Mwanao anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ………………………… bila kukosa. Ni muhimu mwanao kuripoti tarehe hiyo ili ashiriki kikamilifu katika utaratibu ulioandaliwa na shule.

❖ **Mwanao aje na sare kama ifuatavyo:-**

*(i)* Sare za shule hii ni suruali ya **darkbluu** shati jeupe la mikono mifupi na T-shirt ya shule na sweta rangi ya dark blue yenye v-shingoni
**NB:** T.shirt zinapatikana kwenye maduka ya karibu na shule kwa bei ya Tshs. ***15000/= na sweta kwa bei ya Tshs.25000/=.***

(ii) Suruali ya shule inatakiwa iwe na marinda mawili, upana wa chini uwe kumi na nane (18).

(iii) Viatu vyeusi vya ngozi [jozi mbili] vya kamba (**visivyo *na kamba havitapokelewa)*** na soksi nyeusi jozi mbili.

(iv) Sare ya michezo kwa shule hii ni Bukta ya bluu na T.shirt ya blue na Raba (Rubber shoes.)

(v) ***Nguo za nyumbani haziruhusiwi kabisa.*** Hivyo, Mwanafunzi aje na **Suruali mbili za rangi Nyeusi** kwa ajili ya kushindia, iwe na marinda mawili.

(vi) Matibabu yatakayo tolewa shuleni ni ya huduma ya kwanza ambayo yatatolewa katika zahanati ya shule na yale ya rufaa yatagharamiwa na

mzazi. Mwanafunzi anashauriwa aje na kitambulisho cha bima ya afya kwa matibabu ya rufaa.

***Mwanafunzi atakaye kiuka masharti haya hatapokelewa***

**NB: Maelekezo zaidi juu ya sare za shule wasiliana na ofisi ya malezi 0753592239**

## 2. Mahitaji Muhimu kwa mwanafunzi anavyotakiwa kuja navyo.

(i) Taulo moja (1)
(ii) Chandarua(1)
(iii) Godoro la sponji **moja** futi **mbili na nusu** lenye kava la nailon.
(iv) Mto na foronya mbili ( rangi ya shuka)
(v) Shuka za bluu bahari ( Light blue) (2)
(vi) Sanduku la bati (1)
(vii) Bakuli moja (1)
(viii) Sahani moja (1)
(ix) Ndoo moja (1)
(x) Kijiko kimoja (1)
(xi) Oxford students Dictionary (1)
(xii) Wazazi/Walezi mnashauriwa kuwanunulia watoto wenu vitabu muhimu vya masomo husika.
(xiii) Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba **jozi mbili (2)** na soksi nyeusi jozi mbili (2) zisizo na marembo au maandishi yoyote.
(xiv) **Nguo za michezo**: Jezi ya bluu (bukta na fulana yake) na Raba za michezo
(xv) Picha (**passport size**) moja ya mzazi/mlezi na ya mwanafunzi husika (*mwanafunzi husika picha nne).*
(xvi) Namba za simu za mkononi za wazazi/walezi wa mwanafunzi na anuani za posta.
(xvii) Rubber squezer(01), fagio laini la ndani(Soft broom 01), fagio la nje(Chelewa 02) na sabuni ya chooni dumu la lita 5 moja.

## 3. Sheria na kanuni muhimu za shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya Rais -TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

**1. HESHIMA**

(i) Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kumsalimia mwalimu au mtu yeyote anayemzidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.

(ii) Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha mbaya wakati wote kwa mwalimu na watu wengine.

(iii) Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wafanyakazi wote shuleni walimu na wasio walimu kama walezi

(iv) Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu na kuthamini kazi

(v) Mwanafunzi haruhusiwi kufanya yafuatayo:-
(a) Kuvuta sigara/ulevi/ uasherati
(b) Kufuga kucha ndefu, nywele ndefu na ndevu
(c) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima
(d)Kugombana na kupigana.

(vi) Mwanafunzi aitikie wito mara moja anapoitwa, mathalani kengele ya dharura au anapoitwa na kiongozi

(vii) Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu Bendera ya Taifa, wimbo wa Taifa, picha za Viongozi wa Serikali , nembo ya Taifa na fedha za Taifa.

(viii) Mwanafunzi atatakiwa kuheshimu ukumbi wa mikutano, mahali pa kulia, ofisi za shule, mali binafsi na mali ya umma.

(ix) Mwanafunzi anatakiwa kunyoosha mkono juu na kusimama anapoulizwa au kujibu swali darasani.

(x) Mwanafunzi anatakiwa kukaa kimya wakati wote anapokuwa darasani na asitoke nje bila ya ruhusa ya mwalimu au kiongozi aliyepo.

(xi) Mwanafunzi kuwa au kumiliki simu ya mkononi endapo atakamatwa nayo itaharibiwa.

(xii) Mwanafunzi hataruhusiwa kumiki kifaa chochote kinachotumia umeme.

**4:2 MAHUDHURIO**

(i) Mwanafunzi atatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.

(ii) Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria shughuli zote za elimu ya kujitegemea kama vile Kilimo, ufugaji na bustani.

(iii) Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano yote ya shule kama vile Baraza la shule, ukaguzi wa usafi, kupandisha Bendera ya Taifa, mikutano ya nyumba n.k.

**4:3 MAANDALIO YA JIONI**

(i) Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria maandalio ya jioni kuanzia saa 01:30 usiku mpaka saa 4:00 usiku.

(ii) Mwanafunzi anatakiwa kukaa kimya wakati wote wa maandalio ya jioni hatakiwi kuwa na redio wala majadiliano ya vikundi

## 4:4 KUWAHI

(i) Mwanafunzi anatakiwa kuthamini muda kwa kuwahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa kwenye ratiba ya shule ya kila siku.

## 4:5 SARE YA SHULE

(i) Mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare ya shule ambayo ni:-
- (a) Suruali ya dark bluu iliyokolea
- (b) Shati nyeupe yenye nembo ya shule na yenye mikono mifupi
- (c) Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba na soksi nyeusi

(ii) Sare hii itavaliwa na mwanafunzi wakati wote wa:-
- (a) Masomo ya darasani
- (b) Kutoka nje ya shule kwa shughuli za shule
- (c) Mhadhara wa shule ( Baraza la shule)
- (d) Anapokwenda Hospitalini
- (e) Wanaposafiri kuja na kwenda nyumbani

(iii) Sare na mavazi yanayovaliwa na mwanafunzi shuleni yanatakiwa kuwa safi wakati wote.

## 4:6 MIPAKA YA SHULE

(i) Mwanafunzi ataonyeshwa mipaka ya shule

(ii) Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila kibali maalum

(iii) Mwanafunzi itabidi apate kibali maalum kama itabidi alale nje ya shule

(iv) Mwanafunzi haruhusiwi kutembea sehemu zifuatazo bila sababu maalum:-
- (a) Chumba cha walimu ( Staffroom)
- (b) Ofisi za shule
- (c) Maabara
- (d) Jikoni
- (e) Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu

(v) Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kutembelea sehemu zifuatazo:-
- (a) Vilabu vya pombe
- (b) Majumba ya starehe
- (c) Majumba ya kufikia wageni

(vi) Mwanafunzi haruhusiwi kufanya shughuli yoyote katika nyumba ya Ibada (mfano kula, kulala, kusoma n.k) isipokuwa kuabudu tu kwa wakati maalum.

## 4:7 USAFI

Mwanafunzi azingatie usafi wake binafsi na mazingira ya shule kama vile mahali pa kulala (Bwenini) , vyoo, madarasa na maeneo yote yanayozunguka shule.

## 4:8 UKUMBI WA CHAKULA

(i) Mwanafunzi anatakiwa kula chakula katika ukumbi wa chakula na si sehemu nyingine yoyte, Wakati wa kula anapaswa kuwa ameketi chini.
(ii) Mwanafunzi atalazimika kufanya usafi siku ya zamu yake katika ukumbi wa chakula, maeneo ya ukumbi na vyombo vya kupakulia chakula.
(iii) Mwanafunzi haruhusiwi kula chakula jikoni.
(iv) Mwanafunzi anatakiwa kuvaa nguo za heshima anapoingia ukumbi wa chakula, ni marufuku kuingia na taulo, mswaki, bukta n.k.

## 4:9 BWENINI

(i) Kila mwanafunzi atawajibika kufanya usafi kila siku katika eneo atakalopangiwa na kiongozi wake.
(ii) Mwanafunzi lazima awepo kwenye ukaguzi wa jumamosi
(iii) Mwanafunzi haruhusiwi kumkaribisha mgeni yeyote katika mabweni wakati wote
(iv) Magari hayaruhusiwi kuingia katika sehemu ya mabweni
(v) Mwanafunzi atatakiwa kutunza mali aliyokabidhiwa bwenini na kuirejesha kila mwisho wa muhula.
(vi) Ni marufuku kupeleka viti, meza na chakula bwenini.

## 4:10 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

(i) Wizi
(ii) Uasherati, ubakaji na ushoga
(iii) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
(iv) Uvutaji wa bangi
(v) Makosa ya jinai
(vi) Kupigana au kupiga
(vii) Kuharibu makusudi mali ya Umma
(viii) Kudharau Bendera ya Taifa
(ix) Kutoka nje ya shule bila kibali
(x) Kuoa au kuolewa
(xi) Kusababisha mimba ndani na nje ya shule
(xii) Kuchochea kutoa mimba
(xiii) Kugoma, kuchochea, kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
(xiv) Kukataa adhabu kwa makusudi
(xv) Tabia ya utoro hata baada ya kuonywa
(xvi) Kutohudhuria shuleni kwa siku 90 mfululizo
(xvii) Kumiliki simu

**4. Mambo mengine muhimu:-**

(i) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa ***Hospitali ya Serikali***. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara atakaporipoti Shuleni.

(ii) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi / mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(iii) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na Shule.

(iv) Wasilisha kivuli cha cheti cha kuzaliwa

Tafadhali soma kwa makini maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

Shule ya Sekondari Pugu iko mkoa wa Dar es salaam- Wilaya ya Ilala. Ukifika kituo cha mabasi ya mikoani Mbezi (Magufuli bus terminal), panda magari ya kwenda Gongolamboto. Teremka Gongo la mboto, panda gari inayokwenda Kigogo Fresh au Chanika , teremka kituo cha Pugu Sekondari.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**MKUU WA SHULE**

**Fomu maalum ya ukaguzi wa ukamilifu wa mahitaji muhimu**

Jina la Mwanafunzi ----------------------------------------darasa -----------tarehe ya

Ukaguzi---------------------------------------------

1. Mahitaji muhimu mengineyo

(i) Viatu vyeusi jozi mbili
(ii) Soksi nyeusi jozi mbili
(iii) Bukta rangi ya bluu moja .
(iv) Taulo moja
(v) Godoro la sponji
(vi) Sanduku la chuma
(vii) Shuka mbili za bluu ya mpauko
(viii) Kijiko cha steel kimoja
(ix) Bakuli moja
(x) Soft broom 1
(xi) Chelewa 02
(xii) Sabuni ya maji lita 5 dumu 1
(xiii) Rubber squezer........1
(xiv) Sahani moja
(xv) Ndoo moja
(xvi) Rubber shoes jozi moja

2. Cheti cha kuzaliwa (copy)
3. Fomu ya uchunguzi wa afya ya mwanafunzi (Medical examination form)
4. fomu ya maelezo binafsi
5. fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria za shule.

Jina la mkaguzi ......................................................................

Sahihi ya mkaguzi ..................................................

***Muhimu: mwanafunzi hatapokelewa shuleni iwapo fomu hii haitakamilika.***

**FOMU NA 1**

**NAFASI YA KUENDELEA NA MASOMO YA SEKONDARI**

Mwanafunzi ……………………………………………kidato cha …….mwaka ………………

Nimefurahi kupokea nafasi iliyotajwa hapo juu aliyopewa mwanangu na nimeafiki kuwa aipokee. Nitajitahidi kumtimizia mahitaji ya muhinu kulingana na miongozo ya shule. Wakati wote nitakuwa tayari kusaidiana na uongozi wa shule katika kumlea kijana wangu.

Mimi……………………………………………………(Jina kamili )

Umri………….Kijiji ……………………………Wilaya ya……………………………….

Dini ………………………………Uraia……………………………Kazi …………………………

SAINI…………………………..

**3.MWENYEKITI / KATIBU WA KIJIJI**

Nathibitisha kuwa yote yaliyoandikwa na Mwanafunzi (jina)…………………………

na Mzazi/ Mlezi (jina) ……………………………………………………………

Sahihi…………………………………

Mhuri …………………………………

**FORM NO. II**

**DAR ES SALAAM CITY COUNCIL**
**STUDENT MEDICAL CERTIFICATE**

**(TO BE COMPETED BY GOVERNMENT MEDICAL OFFICER AND RETURNED TO THE HEADMASTER OF PUGU SECONDARY SCHOOL)**

**FROM…………………………………………………**

**Re:……………………………………………………………Age……………………..**
**Please examine the above named student and comment on his health by responding to the following items. Kindly put a tick in form of either YES or NO.**

**A. Does the student have problems in connection with**

**SIGHT** (i) YES
(ii) NO
**If YES state ………………………………………………………………………….**
**HEARING** (i) YES
(ii) NO

**If YES state…………………………………………………………………………..**
**SPEECH** (i) YES
(ii) NO
**If YES state ………………………………………………………………………….**
**T.B** (i) YES
(ii) NO

**If YES state ………………………………………………………………………….**
**BLOOD PRESSURE** (i) YES
(ii) NO

**If YES state…………………………………………………………………………..**
**ANY PHYSICAL DISABILITY** (i) YES
(ii) NO

**If YES state…………………………………………………………………………**
**STOOL** (i) YES
(ii) NO
**If YES state …………………………………………………………………………..**
**ANY OTHER FINDINGS ……………………………………………………………….**

**B. DOCTOR'S RECOMMENDATION ……………………………………………………**

| | | |
|---|---|---|
| ……………………………… | ……………………………………… | …... ………………… |
| ***Name and signature*** | ***Designation*** | ***Station*** |